

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA

# JARIDA LA KOROSHO KUANZIA DESEMBA 15 - 31, 2022



VOL. 1 CBT.Na.0005

Imeandaliwa na:
Bodi ya Korosho Tanzania

## 1.0 UTANGULIZI

Kipindi cha mavuno na masoko nchini kinaelekea ukingoni kwa mikoa ya kusini, huku kalenda ya mwaka ya zao ikionesha ni muda wa kumaliza maandalizi ya shamba jipya, kupandikiza miche shambani, kupanda mbegu bora na kupanda mazao mchanganyiko ili kupata tija katika uwekezaji kwenye zao la korosho. Shughuli hizi zinaenda sambamba na mauzo ya korosho katika nchi wanunuzi ambayo hufanyika katika kipindi chote cha mwaka kwa kuzingatia mahitaji na uwepo wa korosho katika soko.

## 2.0. MWENENDO WA SOKO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI

### 2.1. Mwenendo wa soko Msumbiji

Kwa mujibu wa mwenendo wa masoko katika nchi za India na Vietnam katika wiki za mwishoni mwa mwezi Disemba, 2022, bei za korosho ghafi kutoka nchi ya Msumbiji kwa soko la India na Vietnam hazina mabadiliko makubwa na bei za wiki za mwanzo za mwezi Disemba, 2022. Korosho ghafi zimeuzwa kati ya dola za Kimarekani 1,125 hadi 1,150 kwa tani kwa ubora wa "SHOT" 47 hadi 48 (Cashewinfo).

### 2.2. Hali ya Soko la Korosho Nchini India

Katika soko la India mahitaji ya korosho karanga hayana mabadiliko, huku sikukuu kubwa za ufungaji wa ndoa zikikaribia ambazo zinatarajiwa kuanza wiki ya tatu ya mwezi Januari, 2023. Korosho ghafi kutoka Tanzania zimeanza kuingia katika bandari ya Mangarole zenye ubora wa SHOT 52/53, huku kiasi kikubwa kikitarajiwa kupokelewa mwezi wa Januari.
Bei za korosho ghafi katika soko la India ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 2

### 2.3. Hali ya Soko la Korosho katika Nchi ya Vietnam

Katika mwaka 2022, nchi ya Vietnam inakadiriwa kusafirisha wastani wa tani 520,000 za korosho karanga (cashew kernel) ambacho ni pungufu ukilinganisha na kiasi cha tani 580,000 kilichosafirishwa msimu wa 2021 (Cashewinfo). Kwa miaka mitatu mfululizo nchi hii imeendelea kuwa kinara katika ubanguaji duniani na imefanikiwa kusafirisha zaidi ya tani 500,000 za korosho karanga kila mwaka zenye thamani zaidi ya dola za Kimarekani billion tatu (3).
Soko la korosho karanga limeendelea kuwa na uhaba wa korosho karanga za madaraja ya W180, W210, na W240 katika soko la Vietnam kwa sasa, hivyo wanunuzi waliopo wanaendelea kusubiri mazao mapya mwishoni mwa mwezi Machi, 2023 wakati wa msimu wa mavuno nchini Vietnam.

### 2.4. Uzalishaji wa korosho duniani kwa mwaka 2022

Katika mwaka 2022, nchi ya Ivory Coast imeendelea kuwa kinara wa uzalishaji wa korosho duniani ambapo imezalisha wastani wa tani 1,020,000 za korosho ghafi. Nchi ya Cambodia ambayo imeibuka hivi karibuni kuwa na uzalishaji mkubwa inakadiriwa kuzalisha wastani wat ani 750,000 ambazo ni pungufu ukilinganisha na wastani wat ani 1,150,000 zilizozalishwa mwaka 2021. India na Vietnam kwa pamoja zinakadiriwa kuzalisha tani 975,000 hadi 1,000,000 ambayo ni pungufu kwa tani 100,000 hadi 150,000 ukilinganisha na msimu 2021. Makadirio ya Uzalishaji kwa nchi 14 zinazochangia kiasi kikubwa cha uzalishaji duniani ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 1

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa korosho duniani**

| MAKADIRIO YA UZALISHAJI KATIKA NCHI MBALIMBALI KWA MSIMU 2022 | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **Nchi** | **Uzalishaji (Tani)** |
| 1 | Ivory Coast | 1,020,000 |
| 2 | Ghana | 180,000-200,000 |
| 3 | Cambodia | 750,000 |
| 4 | Benin | 180,000 |
| 5 | Nigeria | 210,000 |
| 6 | Guinea Bissau | 200,000-210,000 |
| 7 | Gambia and Senegal | 65,000-70,000 |
| 8 | Togo | 30,000 |
| 9 | Msumbiji (2022/2023) | 153,000 |
| 11 | Guinea/Mali/Magadascar | 95,000-105,000 |
| 12 | Indonesia | 130,000-150,000 |
| 13 | Vietnam/India | 975,000-1,000,000 |
| 14 | Brazil | 130,000-150,000 |
| | **Jumla Kuu** | **4,338,000- 4,453,000** |
| | **Chanzo: Cashewinfo** | |

**Jedwali Na.2: Bei za korosho ghafi katika nchi ya India na Vietnam hadi 31 Disemba,2022**

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI (RCN) DUNIANI-CASE STUDY YA INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DESEMBA, | | |
|---|---|---|
| **TAREHE** | **BEI-CIF USD/TON** | |
| | **BEI YA CHINI** | **BEI YA JUU** |
| 31 Oktoba, 2022 | 1,050 | 1,280 |
| 27 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 12 Disemba, 2022 | 1,100 | 1,330 |
| 24 Disemba, 2022 | 1,150 | 1,320 |
| 31 Disemba, 2022 | 1,125 | 1,320 |
| SOT: 48-52 | | |




**Chanzo: Cashewnutinformation**

## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

## 3.1 Bei Ya Korosho Karanga Vietnam Kufikia 31 Disemba, 2022

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini ukilinganisha na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Jedwali Na. 3 linaonesha bei ya korosho karanga hadi kufikia mwishoni mwa Disemba, 2022.

**Jedwali Na. 3**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA 31 DISEMBA, 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | WW180 | 7.82 | 8.15 | 18,142.40 | 18,908.00 |
| White Whole Cashews 210 | WW210 | 7.05 | 7.27 | 16,356.00 | 16,866.40 |
| White Whole Cashews 240 | WW240 | 5.84 | 6.28 | 13,548.80 | 14,569.60 |
| White Whole Cashews 320 | WW320 | 5.51 | 5.84 | 12,783.20 | 13,804.00 |
| Large Pieces | LP | 3.52 | 4.30 | 8,166.40 | 9,976.00 |
| Small Pieces | SP | 2.97 | 3.30 | 6,890.40 | 7,656.00 |

**Chanzo:** Cashewinformation
*Exchange Rate: 1USD = TZS 2,320 (BOT)*

## 3.2 Bei Ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Hadi Kufikia 31 Disemba, 2022

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Disemba, 2022 makadirio ya bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni Ivory Coast, Ghana, Benin, Guinea Bissau nk. ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 4**

**Jedwali Na. 4**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA 31 DISEMBA, 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | | | | |
| White Whole Cashews 210 | W210 | 7.599 | 7.930 | 17,629.68 | 18,397.60 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.947 | 6.278 | 13,797.04 | 14,564.96 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.617 | 5.837 | 13,031.44 | 13,541.84 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.176 | 5.507 | 12,008.32 | 12,776.24 |
| White Splits | WS | 4.185 | 4.736 | 9,709.20 | 10,987.52 |
| Large Pieces | LP | 3.194 | 3.414 | 7,410.08 | 7,920.48 |
| Small Pieces | SP | 2.643 | 2.863 | 6,131.76 | 6,642.16 |

**Chanzo:** Cashewinformation
*Exchange Rate: 1USD = TZS 2,320 (BOT)*

## 3.4 Bei Ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje Ya Nchi Hadi Kufikia 31 Disemba, 2022

Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje ya nchi hazina mabadiliko kufikia mwishoni mwa Disemba, 2022 kama inavyoonesha jedwali Na. 5. Aidha uwiano wa bei kwa madaraja tofauti ya korosho karanga umeendelea kuonyesha nchi ya Vietnam kuwa na bei ndogo ukilinganisha na nchi za Afrika, huku Tanzania ikionekana kuwa na bei ya juu ya korosho karanga.


**Jedwali Na.5**

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA 31 DISEMBA, 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | 8.00 | 8.30 | 18,560.00 | 19,256.00 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 7.20 | 7.50 | 16,704.00 | 17,400.00 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 6.80 | 7.10 | 15,776.00 | 16,472.00 |
| White Splits | WS | 4.50 | 5.10 | 10,440.00 | 11,770.80 |
| Large White Pieces | LWP | 3.50 | 4.20 | 8,120.00 | 9,693.60 |

**Chanzo:** TACP
*Exchange Rate: 1USD = TZS 2,320 (BOT)*

### Jedwali Namba 6: Uwiano Wa Bei Daraja WW320

| UWIANO WA BEI DARAJA LA WW320 FOB | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Nchi | Bei ya Chini Dola/Kilo | Bei ya Juu Dola/Kilo | Bei ya Chini Tzs/Kilo | Bei ya Juu Tzs/Kilo |
| Vietnam | 5.51 | 5.95 | 12,783.20 | 13,804.00 |
| Afrika Magharibi | 5.62 | 5.84 | 13,038.40 | 13,548.80 |
| Tanzania | 6.80 | 7.10 | 15,776.00 | 16,472.00 |




## 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2022 jumla ya tani 167,919.978 tayari zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada kwa thamani ya shilingi 314,265,029,035. Minada ya mauzo ya korosho bado inaendelea katika maeneo mbalimbali nchini, huku mikoa ya kusini ikielekea ukingoni na mikoa ya Tanga, Singida (Manyoni), Iringa n.k ikijiandaa kuanza kuuza korosho zake. Katika wiki ya mwisho mwa Disemba, bei ya chini kwa korosho daraja la kwanza imeshuka kwa asilimia 1.2 kutoka wiki iliyoishia tarehe 15 Disemba ambapo bei ya chini ilikuwa Tshs.1,650 kwa kilo. Bei ya juu imeshuka kwa asilimia 3.1 ambapo katika wiki iliyoishia tarehe 15 Disemba,2022, bei ya juu ilikuwa Tshs. 1,960 kwa kilo. Sababu ya kushuka kwa bei hizi ikiwa ni kupungua kwa ushindani sokoni kwani wanunuzi wengi waliohitaji korosho kwa msimu huu tayari wamekamilisha mahitaji yao na hawashiriki katika minada kwa sasa. Aidha, kushuka kwa ubora katika baadhi ya maeneo ambapo mvua zimeanza kunyesha huku mahitaji makubwa ya korosho ghafi katika nchi wanunuzi yakiendelea kuwa katika ubora wa kuanzia SHOT 50 hadi 54 kwa gunia la kilo 80.

### Jedwali Na. 7a: Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani

| Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani (Desemba 16 hadi Desemba 31) | | |
|---|---|---|
| KIPINDI CHA | KIASI KILICHOUZWA (kg) | THAMANI (TZS) |
| Wiki ya Sasa | 7,074,384 | 12,159,233,338 |
| Jumlishi Wiki Iliyopita | 160,845,594 | 302,105,795,697 |
| Jumla | 167,919,978 | 314,265,029,035 |

### Jedwali Na. 7b: Muhtasari Bei za Mnada wa Kitaifa Korosho Ghafi

| Muhtasari Bei za Mnada wa Kitaifa Korosho Ghafi | | | |
|---|---|---|---|
| Wiki iliyopita (Desemba 07 hadi Desemba 15) | | Wiki ya Sasa (Desemba 16 hadi Desemba 31) | |
| Mwenendo wa Bei | Wiki | Daraja la Kawaida | |
| | | Bei ya Juu (Tshs) | Bei ya Chini (Tshs) |
| | *Bei ya sasa* | 1,900 | 1,630 |
| | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,960 | 1,650 |
| | *Mabadiliko (%)* | ▼3.1% | ▼1.2% |



**Jedwali Na. 7c: Bei ya Mauzo ya Mkoa Korosho Ghafi**

| Bei ya Mauzo Korosho Ghafi ya Mkoa (Desemba 16 hadi Desemba 31) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MKOA | CHAMA KIKUU | WIKI | Daraja la Kawaida | |
| | | | Bei ya Juu (Tshs) | Bei ya Chini (Tshs) |
| MTWARA | MAMCU | *Bei ya sasa* | 1,820 | 1,700 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,920 | 1,700 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼5.2% | ▶0.0% |
| | TANECU | *Bei ya sasa* | 1,800 | 1,750 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,940 | 1,931 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼7.2% | ▼9.4% |
| LINDI | RUNALI | *Bei ya sasa* | 1,900 | 1,756 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,960 | 1,850 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼3.1% | ▼5.1% |
| | LINDI MWAMBAO | *Bei ya sasa* | 1,726 | 1,726 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,726 | 1,726 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▶0.0% | ▶0.0% |
| PWANI | CORECU | *Bei ya sasa* | 1,630 | 1,630 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,707 | 1,650 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼4.5% | ▼1.2% |
| RUVUMA | TAMCU | *Bei ya sasa* | 1,757 | 1,757 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,755 | 1,707 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▲0.1% | ▲2.9% |
| MOROGORO | UKICU | *Bei ya sasa* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,721 | 1,721 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | NA | NA |

Alama (▲▼▶) zinaonyesha mwelekeo wa mabadiliko ya bei. (▲) Bei imeongezeka; (▼) Bei imeshuka;(▶) Hakuna mabadiliko ya bei.

## 5.0 UHAMASISHAJI MATUMIZI NA UWEKEZAJI KATIKA BIDHAA ZA KOROSHO NCHINI

Katika uhamasishaji matumizi ya bidhaa za korosho nchini, katika toleo hili imeainishwa namna ya uandaaji wa Mshikaki ya Mabibo Ya Korosho Maarufu Kama (Mshikaki Wa Korosho). Mshikaki wa Korosho unaandaliwa kama ambavyo unaandaliwa mshikaki mwingine wa nyama ya ng'ombe au kuku.

### 5.1. Mahitaji

i. Unahitaji vitu vifuatavyo ili kupata mshikaki bomba wa korosho
ii. Mabibo 8 au zaidi kulingana na idadi ya mishikaki utakayohitaji (Mabibo yawe yamekomaa vizuri, yasiwe yamevunwa muda mrefu kabla ya uandaaji)
iii. Vitunguu viwili vilivyokatwa katwa vipande vya wastani
iv. Pilipili mbili za kijani zilizokatwa katwa vipande vya wastani
v. Nyanya 4 zilizokatwa mara 4 kila moja
vi. Vitungu swaumu vilivyomenywa na kupondwa
vii. Vijiko viwili vya mafuta ya kula (inashauriwa mafuta ya karanga)
viii. kiungo cha ngo'mbe moja kijiko 1 (Beef seasoning)

ix. Pilipili kavu (Chill Powder) kijiko kimoja cha chai
x. Pilipili Manga kijiko kimoja cha chai
xi. Chumvi ya mezani kijiko kimoja
xii. Haradali (mustard) gramu 50
xiii. Gramu 50 ya unga wa korosho

**5.2. Jinsi ya Kuandaa:**

i. Menya na ukate mabibo ya korosho kwa vipande vya mche mraba (kama umbo la mshikaki wa ng'ombe);
ii. Chemsha vipande katika lita moja ya maji kwa dakika 10;
iii. Chuja kisha acha ipoe;
iv. Andaa viungo vyako (marinade) na uchanganye vitunguu swaumu, viungo vya nyama (beef seasoning), pilipili manga, chumvi, haradali, siki (vinegar) na unga wa korosho;
v. Kisha weka vipande vya mabibo ulivyokwisha chemsha kwenye viungo ulivyoandaa (mari nade);
vi. Weka vipande vya mabibo ya korosho, pili pili ya kijani, vipande vya nyanya na pili pili hoho vyote chomeka kwenye kijiti cha kuchomea mshikaki (Pangilia kwa umaridadi);
vii. Kisha choma kwenye moto wa joto la wastani kwa dakika 3 hadi 5;
viii. Tayari kwa Kula na Saladi.



chanzo:Akros Ltd

**Mishikaki ya korosho mbadala sahihi wa mshikaki wa kuku/ng'ombe**

**MAWASILIANO**
**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
**S.L.P 533 TANU ROAD – MTWARA**
**Simu: +255 (23) 233 3303/233 3450**
**Barua pepe: info@cashew.go.tz**
**Tovuti: www.cashew.go.tz**